

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO

08 JUNI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO – TAREHE 08 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

530. MHESHIMIWA YAGI MAULID KIARATU (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza Bajeti ya TARURA Manispaa ya Singida kwa kuwa ni ndogo.

WIZARA YA KILIMO:

531. MHESHIMIWA ONESMO MERDSON MNKONDYA (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha uuzaji wa Mbegu feki nchini.

532. MHESHIMIWA KUNTI YUSUPH MAJALA (CHEMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itakarabati Skimu ya Umwagiliaji katika Kijiji cha Jogolo, Kata ya Ovada - Chemba.

533. MHESHIMIWA ENOCK ZADOCK KOOLA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Soko kubwa la Kimataifa la Mazao katika eneo la Lokolova ili kunufaika na ukaribu wa mpaka wa Kenya.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

534. MHESHIMIWA ASHA JUMA KOMBO (MFENESINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wahitimu wa Vyuvo vya VETA nchini wanapata ajira au fursa za kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo yao.

WIZARA YA UJENZI:

535. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Bombo Mtoni - Umba hadi Mkomazi ambayo ipo kwenye Ilani ya CCM utaanza.

536. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza rasmi ujenzi wa Barabara ya Mbalizi hadi Mkwajuni.

537. MHESHIMIWA ENG. JOHNSTON JOHANSEN MUTASINGWA (BUKOBA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Njia Nne katika Barabara ya Rwamishenye – Kastamu yenye urefu wa km 1.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

538. MHESHIMIWA IBRAHIM MOHAMED SHAYO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itakitambua Chama cha Wapagazi - *Tanzania Association of Posters* (TAP) na kukishirikisha kama Mdau muhimu wa Utalii nchini.

WIZARA YA NISHATI:

539. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, hadi sasa ni Vitongoji vingapi vilivyopatiwa umeme katika Jimbo la Tarime Vijini.

540. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini umeme utafika kwenye Mitaa yote ambayo haina umeme katika Mji wa Tarime.

**DODOMA
08 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**